

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA SHIRIKA LA  
CHILDREN'S DIGNITY FORUM (CDF) – JUKWAA LA UTU WA MTOTO  
KIPINDI CHA ROBO YA PILI YA MWAKA (Oct 2018 – Des 2018)**

<b>S/N</b>	<b>Shughuli iliyofanyika</b>	<b>Wanufaika</b>
1	Mafunzo ya haki za watoto, stadi za maisha, mifumo ya rufaa kwa Wasichana wanachama wa Klabu za CDF shule za Msingi na Sekondari	Wasichana 480 walifikiwa kutoka shule za 7 za Sekondari na 9 za Msingi kutoka kata za Mpwapwa Mjini, Kibakwe, Pwaga na Berege.
2	Mafunzo ya afya ya uzazi kwa wasichana wanachama wa Klabu za CDF za shule za Msingi na Sekondari	Wasichana 155 walifikiwa kutoka shule za 7 za Sekondari na 9 za Msingi kutoka kata za Mpwapwa Mjini, Kibakwe, Pwaga na Berege.
3	Bonanza la michezo kuhamasisha ushiriki wa wanaume katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto	Waendesha bodaboda 20 (Wanaume) na Wanachama 43 (8F, 35M) wa Kikundi cha Malezi Berege walifikiwa na mafunzo ya nafasi ya wanaume kukomesha ukatili wa kijinsia huku zaidi ya wananchi 400 wakihudhuria Bonanza na kufikiwa na ujumbe wa haki za wanawake na watoto na nafasi ya mwanaume katika kuleta usawa wa kijinsia
4	Mkutano wa Mwaka wa Wilaya wa Wadau wa Haki za Mtoto Wilayani Mpwapwa	Wajumbe 49 (20 F, 29 M) walihudhuria na kujadili hali ya ulinzi wa mtoto kiwilaya, changamoto za kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto pamoja na kuweka mikakati ya pamoja katika kukabiliana na aina zote za ukatili dhidi ya watoto.
5	Ushiriki wa Kongamano la Kitaifa la kukabiliana na Ndoa za Utotoni, Mimba za Utotoni na Ukeketaji pamoja na Kongamano la Sauti za Wasichana (Girls Voice Forum)	Jumla ya Wasichana 10 kutoka Mpwapwa Walishiriki kongamano la Kitaifa la kukabiliana na Ndoa za Utotoni, Mimba za Utotoni na Ukeketaji ambalo lilifanyika hotel ya Serena Dar e salaam. Pia jumla ya Wasichana 20 walihudhuria Kongamano la Sauti za Wasichana lililofanyika Chuo Kikuu cha Ualimu Dar es salaam (DUCE).
6	Tathmini ya shughuli za kiuchumi/ujasiriamali (income generating /entrepreneurship activities) kwa wasichana kutoka kata za Mpwapwa Mjini, Kibakwe, Berege na Pwaga	Wasichana 42 wajumbe wa Klabu za Wasichana wan je ya shule wamefanyiwa tathmini ya shughuli za ujasiriamali wanazotaka kuzifanya. CDF inatarajia katika kipindi cha kati ya Januari hadi Machi 2019 kuwawezesha wasichana hawa kuanzisha shughuli za uchumi/ujasiriamali ili kujipatia kipato.